MAJIBU NA NASAHA ZA AHLUL-‘ILM NA MASHAYIKH

KUHUSU DAWRA IJAYO YA “MASHAYIKH WA ADEN.”

أجوبة ونصائح أهل العلم والمشايخ حول الدورة القادمة لمشايخ عدن.

SDEA

JAWABU NA NASAHA ZA AS-SHAYKH AL-MUHADDITH BILAL AS-SAALIMIY (hafidhahullah).

Alhamdulillah.

Wa 'alaykumus-Salaam wa Rahmatullahi wa Barakaatuh.

Hayyakumullah Allahawabariki, na atujaalie sisi na nyinyi tufuate haki na tudumu juu yake.

Ama kuhusu **dawrah hii, waandaaji wake na Masheikh wanaoshiriki ndani yake**, jambo hili si suala la kawaida linaloweza kupuuzwa kwa kisingizio tu kwamba ni **dawrah** ya ki-ilmu, au kwa sababu jina lake linahusishwa na **Imamu Ash-Shaafi'iy** رحمه الله.

Kwa hakika, jambo la kuzingatiwa si majina wala vichwa vya habari, bali ni **uhalisia wa Masheikh hawa waliotajwa, ilmu na manhaj wanayobeba, pamoja na yale wanayoyasambaza miongoni mwa wanafunzi.**

Na Salafiy anapotaka kuchukua dini na ilmu yake kutoka kwa mtu fulani, haangalii wingi wa darsa, wala uzuri wa uwasilishaji, wala umaarufu; bali huangalia **usahihi wa itikadi na manhaj, misimamo ya mtu huyo wakati wa fitna, na kiwango cha kuafikiana kwake na Kitabu na Sunnah pamoja na yale waliyokuwa nayo Salaf wa Ummah.**

Miongoni mwa mambo hatari ambayo yanapaswa kutiliwa mkazo katika qadhia hii ni **yale yaliyothibiti kuhusu misimamo ya Masheikh hawa inayohusiana na kufanya khuruj (uasi) dhidi ya waliyul-amr (mtawala), kuunga mkono miradi (projects) inayosababisha kuvunjwa kwa utiifu na kuzushwa kwa mifarakano, pamoja na juhudi au uungaji**

mkono wa mradi wa kuigawa Yemen na kuitenganisha Kusini yake na Kaskazini yake.

Haya si mambo ya kisiasa ya pembeni kama baadhi ya watu wanavyoweza kuyawasilisha, bali yanahusiana na **misingi mikubwa ambayo Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah wameieleza katika mlango wa kusikia na kutii mtawala, kushikamana na jamaa'h, kuharamisha khuruj/uasi dhidi ya watawala, kutahadharisha dhidi ya fitna, na kukataza kuigawa jamaa'h ya Waislamu na kuvunja utiifu kwa mtawala.**

Allah Taa'laa amesema:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ أَطِيعُواْ ٱللَّهَ وَأَطِيعُواْ ٱلرَّسُولَ وَأُوْلِي ٱلۡأَمۡرِ مِنكُمۡۖ﴾ [النساء: 59]

"Enyi mlioamini! Mtiini Allah, na mtiini Mtume, na wenye mamlaka miongoni mwenu." [An-Nisaa: 59]

Na Mtume صلى الله عليه وسلم amesema:

«مَنْ أَطَاعَنِي فَقَدْ أَطَاعَ الله، وَمَنْ عَصَانِي فَقَدْ عَصَى الله، وَمَنْ يُطِعِ الْأَمِيرَ فَقَدْ أَطَاعَنِي، وَمَنْ يَعْصِ الْأَمِيرَ فَقَدْ عَصَانِي»

"Yule anayenitii, kwa hakika amemtii Allah; na yule anayeniasi, kwa hakika amemuasi Allah. Na yule anayemtii mtawala, kwa hakika amenitii; na yule anayemuasi mtawala, kwa hakika ameniasi."

-Imepokelewa na Al-Bukhari na Muslim.

Na amesema (Mtume) صلى الله عليه وسلم:

«مَنْ أَتَاكُمْ وَأَمْرُكُمْ جَمِيعٌ عَلَى رَجُلٍ وَاحِدٍ، يُرِيدُ أَنْ يَشُقَّ عَصَاكُمْ، أَوْ يُفَرِّقَ جَمَاعَتَكُمْ، فَاقْتُلُوهُ»

"Yeyote atakayekujieni hali ya kuwa jambo lenu limekusanyika chini ya mtu mmoja, akitaka kuvunja umoja wenu au kuitenganisha jamaa'h yenu, basi muueni."

-*Imepokelewa na Muslim.*

Na amesema Mtume عليه الصلاة والسلام:

«وَمَنْ خَرَجَ مِنَ الطَّاعَةِ، وَفَارَقَ الْجَمَاعَةَ، فَمَاتَ، مَاتَ مِيتَةً جَاهِلِيَّةً»

"Na yeyote atakayetoka katika utiifu wa mtawala na akajitenga na jamaa'h, kisha akafa, amekufa kifo cha kijahiliyyah."

-*Imepokelewa na Muslim.*

Kwa hiyo, mlango huu kwa Ahlus-Sunnah si miongoni mwa mambo yanayofaa kufanywa ni mepesi, wala si miongoni mwa masuala ambayo husemwa: ***"Haya ni maoni ya kisiasa,"*** au ***"Ni tofauti katika ijtihadi."*** Kwa kuwa kinachozungumziwa hapa ni **msingi (asl) mkubwa unaohusiana na umoja wa jamaa'h, kusikia na kutii mtawala katika mambo ya wema (ma'ruf), na kufunga milango ya fitna zinazopelekea kwenye machafuko, kumwagika damu na kusambaratika kwa jamii.**

Kwa hiyo, ikiwa imethibiti kwamba da'i ameshiriki au ameunga mkono mradi unaolenga **kuivunja jamaa'h ya Waislamu, kugawanya nchi na kusambaratisha umoja wake, au kufanya uasi (khuruj) dhidi ya waliyul-amr wa kisheria**, basi hilo ni jambo hatari ambalo haifai twalib-ilmu kulipita bila kulizingatia, wala si sahihi kulishughulikia kwa kauli ya baadhi ya watu isemayo: ***"Tunachukua ilmu kwake na tunaacha manhaj yake."***

Kwa sababu suala hapa si kosa la kawaida katika jambo la kifiqhi, wala si kuteleza katika tawi fulani la dini; bali kinachozungumziwa ni **misimamo ya kimanhaj yenye athari zake katika msingi wa kusikia na kutii mtawala, kushikamana na jamaa'h na kutahadharisha dhidi ya fitna.**

Kwa msingi huo, **nawatahadharisha ndugu zetu Masalafiy katika Afrika Mashariki** wasidanganyike na dawrah hii kwa sababu tu ya jina lake, wala wasidanganyike na Masheikh wanaoshiriki ndani yake au umaarufu wa baadhi yao. Hakika kinachozingatiwa ni **uhalisia wa manhaj, si mvuto wa jina; na hali ya mtu anayejitokeza mbele, si jina la dawrah tu.**

Na ninawapa waandaaji wa dawrah hii nasaha maalumu:

Mcheni Allah Taa'laa, na tahadharini msije mkafanya mimbari za ki-ilmu kuwa njia ya kuwapitisha watu na misimamo inayokwenda kinyume na misingi ya Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah, au kuwafanya tullabul-ilmu kuwa madaraja ya kufikia miradi inayosababisha mifarakano na fitna.

Ndugu zenu wamekwishawanasihi — kama ilivyotajwa katika swali — kwa siri na kwa dhahiri. Basi ikiwa yale mliyoyanasihiwa ni haki, na dalili zake zimethibiti, basi wajibu ni **kurejea kwenye haki, kutubia kosa, na kujitenga na misimamo inayopingana na Sharia'h**, si kung'ang'ania, wala kuchochea

mabishano, wala kugeuza suala la ki-ilmu na kimanhaj kuwa ugomvi wa kibinafsi.

Na ninawaambia ndugu zetu katika **Afrika Mashariki**:

Msifanye kuwadhania watu mema kuwa ni kizuizi cha kuijua haki, wala msifanye wingi wa darsa au umaarufu wa Masheikh kuwa kipimo cha usalama (wa kimanhaj).

Mtu anaweza kuwa mzungumzaji katika ilmu, akawa na uangalifu katika baadhi ya milango ya Sharia'h, **lakini wakati huo huo akaangukia katika makosa makubwa katika mlango wa manhaj.**

Ndiyo maana **Salaf** رحمهم الله walikuwa wakizingatia na kuchunguza sana ni nani anayechukuliwa kwake ilmu.

Muhammad bin Siiriin رحمه الله amesema:

«إِنَّ هَذَا الْعِلْمَ دِينٌ، فَانْظُرُوا عَمَّنْ تَأْخُذُونَ دِينَكُمْ»

"Kwa hakika, ilmu hii ni dini; basi chunguzeni mnachukua kwa nani dini yenu."

Imamu Muslim رحمه الله amenukuu kauli hii katika utangulizi wa **Sahih yake**, katika muktadha wa kubainisha wajibu wa kupokea riwaya kutoka kwa watu waaminifu na kuwaacha watu wenye tuhuma na uongo — **kama hali ya Masheikh hawa waliotajwa.**

Na hili ni miongoni mwa mambo makubwa yanayoonyesha kwamba **suala la kuchukua ilmu kutoka kwa watu si suala la hisia, bali ni amana ya kidini.**

Na Allah ndiye Mjuzi zaidi."

MUKHTASARI/SUMMARY:

1. **Kinachozingatiwa si majina wala vichwa vya habari, bali ni uhalisia wa Masheikh hao, ilm na manhaj wanayobeba.**

2. **Salafiy anapotaka kuchukua dini na ilm yake, huangalia usahihi wa itikadi na manhaj, misimamo ya mtu wakati wa fitna, na kufuata Kitabu, Sunnah na yale ya Salaf wa Ummah.**

3. **Miongoni mwa mambo yao hatari ni; khuruj dhidi ya mtawala na kuunga mkono miradi inayosababisha kuvunjwa kwa utiifu kwa watawala na mifarakano; haya ni kinyume na Usuli za Sunah za; Kusikia na kutii mtawala, Kushikamana na jamaa'h na Kutahaharisha dhidi ya fitna.**

4. **Wanatadharishwa ndugu zetu Masalafiy katika Afrika Mashariki wasidanganyike na dawra hii kwa sababu ya jina lake au umaarufu wa Masheikh.**

5. **Na kwa wasimamizi; wamche Allah na wasifanye mimbari za kielimu njia ya kupitisha misimamo inayokwenda kinyume na misingi ya Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah.**

6. **Ikiwa mliyoyanasihiwa ni haki na dalili zake zimethibiti, wajibu ni kurejea kwenye haki, kutubia kosa na kujitenga na misimamo inayopingana na Sharia.**

7. **Kuchukua elimu kutoka kwa watu si suala la hisia, bali ni amana ya kidini (kwa hiyo usiisaliti amana hii ewe salafi).**

الحمد لله:

وعليكم السلام ورحمة الله وبركاته.

حياكم الله، وبارك الله فيكم، ووفقنا وإياكم للحق والثبات عليه.

أما ما يتعلق بهذه الدورة والقائمين عليها والمشايخ المشاركين فيها، فالأمر ليس أمرًا عارضًا يمكن تجاوزه بمجرد كونها دورة علمية، أو لأن عنوانها مرتبط بالإمام الشافعي رحمه الله؛ فإن العبرة ليست بالأسماء والعناوين، وإنما بحقيقة هؤلاء المشايخ المذكورين، وما يحملونه من علم ومنهج، وما ينشرونه بين الطلاب.

والسلفي إذا أراد أن يأخذ دينه وعلمه عن شخص، فإنه لا ينظر إلى كثرة الدروس، ولا إلى حسن العرض، ولا إلى الشهرة، وإنما ينظر إلى سلامة الاعتقاد والمنهج، وإلى مواقف الرجل عند الفتن، وإلى مدى موافقته للكتاب والسنة وما عليه سلف الأمة.

ومن أخطر ما ينبغي التنبيه عليه في هذه القضية ما ثبت عن هؤلاء المشايخ من مواقف تتعلق بالخروج على ولي الأمر الشرعي، ومناصرة مشاريع تؤدي إلى شق عصا الطاعة وإثارة الفرقة، والسعي أو المساندة لمشروع تقسيم اليمن وفصل جنوبه عن شماله.

وهذه ليست مسائل سياسية هامشية كما قد يصورها بعض الناس، بل تتعلق بأصول عظيمة قررها أهل السنة والجماعة في باب السمع والطاعة، ولزوم الجماعة، وتحريم الخروج على ولاة الأمور، والتحذير من الفتن، والنهي عن تفريق جماعة المسلمين وشق عصا الطاعة.

قال الله تعالى:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولِي الْأَمْرِ مِنْكُمْ﴾ [النساء: 59].

وقال النبي صلى الله عليه وسلم:

«مَنْ أَطَاعَنِي فَقَدْ أَطَاعَ الله، وَمَنْ عَصَانِي فَقَدْ عَصَى الله، وَمَنْ يُطِعِ الْأَمِيرَ فَقَدْ أَطَاعَنِي، وَمَنْ يَعْصِ الْأَمِيرَ فَقَدْ عَصَانِي» متفق عليه.

وقال صلى الله عليه وسلم:

«مَنْ أَتَاكُمْ وَأَمْرُكُمْ جَمِيعٌ عَلَى رَجُلٍ وَاحِدٍ، يُرِيدُ أَنْ يَشُقَّ عَصَاكُمْ، أَوْ يُفَرِّقَ جَمَاعَتَكُمْ، فَاقْتُلُوهُ» رواه مسلم.

وقال عليه الصلاة والسلام:

«وَمَنْ خَرَجَ مِنَ الطَّاعَةِ، وَفَارَقَ الْجَمَاعَةَ، فَمَاتَ، مَاتَ مِيتَةً جَاهِلِيَّةً» رواه مسلم.

فهذا الباب عند أهل السنة ليس من الأمور التي يتساهل فيها، ولا من المسائل التي يقال فيها: هذه وجهة نظر سياسية، أو اختلاف في الاجتهاد؛ إذ إن الكلام على أصل عظيم يتعلق بوحدة الجماعة، والسمع والطاعة في المعروف، وسد أبواب الفتن التي تفضي إلى الفوضى وسفك الدماء وتمزيق المجتمعات.

ولهذا فإن ثبوت مشاركة الداعية أو تأييده لمشروع يهدف إلى شق جماعة المسلمين، أو تفريق البلاد وتمزيق وحدتها، أو الخروج على ولي الأمر الشرعي، أمر خطير ينبغي ألا يمر على طالب العلم مرور الكرام، ولا يصح أن يعالج بمثل قول بعض الناس: «نأخذ عنه العلم ونترك منهجه».

فليست القضية هنا مجرد خطأ في مسألة فقهية، ولا زلة في باب من أبواب الفروع، وإنما الكلام في مواقف منهجية لها آثارها على أصل السمع والطاعة ولزوم الجماعة والتحذير من الفتن.

ومن هنا فإنني أحذر الإخوة السلفيين في شرق أفريقيا من الاغترار بهذه الدورة لمجرد عنوانها، أو الاغترار بالمشايخ المشاركين فيها أو شهرة بعضهم؛ فإن العبرة بحقيقة المنهج، لا ببريق العنوان، وبحال المتصدر، لا بمجرد اسم الدورة.

وأخص القائمين على هذه الدورة بالنصيحة:

اتقوا الله تعالى، واحذروا أن تجعلوا المنابر العلمية وسيلة لتمرير الأشخاص والمواقف التي تخالف أصول أهل السنة والجماعة، أو أن تجعلوا طلاب العلم جسورًا للوصول إلى مشاريع تفضي إلى الفرقة والفتنة.

وقد نصحكم إخوانكم ـ كما ذكر في السؤال ـ سرًا وعلنًا، فإن كان ما نُصحتم به حقًا، وثبتت بيناته، فالواجب الرجوع إلى الحق، والتوبة من الخطأ، والبراءة من المواقف المخالفة للشرع، لا المكابرة، ولا التشغيب، ولا تحويل القضية العلمية والمنهجية إلى خصومة شخصية.

وأقول للإخوة في شرق أفريقيا:

لا تجعلوا حسن الظن بالأشخاص يحجبكم عن معرفة الحق، ولا تجعلوا كثرة الدروس أو شهرة المشايخ معيارًا للسلامة.

فقد يكون الرجل متكلمًا في العلم، وله عناية ببعض أبواب الشريعة، ومع ذلك يقع في أخطاء عظيمة في باب المنهج؛ ولهذا كان السلف رحمهم الله شديدي العناية بمن يؤخذ عنه العلم.

قال محمد بن سيرين رحمه الله:

«إن هذا العلم دين، فانظروا عمن تأخذون دينكم».

وذكره الإمام مسلم رحمه الله في مقدمة صحيحه في سياق بيان وجوب الرواية عن الثقات وترك أهل التهم والكذب - كحال هؤلاء المشايخ المذكورين -.

وهذا من أعظم ما يبين أن قضية الأخذ عن الأشخاص ليست قضية عاطفية، وإنما هي أمانة دينية.

والله أعلم.

Ijumaa 15 Rabiu'-l Awwal =28 Aug 2026

الدعوة السلفية شرق إفريقيا

SALAFI DA'WAH EAST AFRICA